



SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

WIZARA YA AFYA

TAARIFA KWA UMMA

MWENENDO WA UGONJWA WA CORONA NCHINI TAREHE 24/04/2020.

Wizara ya Afya, Zanzibar inatoa taarifa ya ongezeko la wagonjwa wapya kumi na tano (**15**) wa Corona (COVID-19) Nchini na kufikia idadi ya wagonjwa tisini na nane (**98**) kutoka themanini na tatu (**83**) ambao tuliowatolea taarifa tarehe 22 Aprili 2020.

Wagonjwa hawa wote ni Raia wa Tanzania, kumi (**10**) kati ya hao wanaishi Unguja na watano (**5**) wanaishi Pemba. Hali ya maambukizi inazidi kungezeka.

Jumla ya maeneo **13** yametengwa Unguja na Pemba, na jumla ya watu **892** wameshawekwa karantin (**624** Pemba na **260** Unguja) katika maeneo hayo hadi sasa. Watu **632** kati yao wamesharuhusiwa baada ya kumaliza muda wa siku **14**, na hakuna aliyejitokeza kuwa na dalili za maradhi haya hadi sasa.

Serikali kupitia wizara ya Afya, inaendelea kuwasisitiza wananchi kuchukua tahadhari zote za kujikinga na ugonjwa huu zinazotolewa mara kwa mara ikiwemo unawaji wa mikono kwa maji yakutiririka na sabuni, kuepuka misongamano na kuahirisha safari za nje na ndani ya nchi zisizo za lazima. Tunawaagiza wananchi wote kuvaa barakoa muda wote wanapotoka nje ya nyumba zao. Utaratibu wa uvaaji na barakoa na aina gani ya barakoa utatolewa na Serikali.

Aidha Wizara inaomba wananchi ambao wana dalili za homa kali, kukohowa na kupiga chafya kujitokeza katika vituo vyetu vya afya au kupiga simu namba 190. Ni vyema mgonjwa mwenye dalili za maradhi haya asijichanganye na wagonjwa au watu wengine na tuache tabia ya kujitibu wenyewe kwani kwa kufanya hivyo tutaendelea kueneza maambukizi na vifo vinavyo husiana na ugonjwa huu.

Pia vyombo vya habari vinahimizwa kupata taarifa za ugonjwa huu wa COVID-19 kutoka Wizara ya Afya.

Ndugu wananchi tuendelee kumuomba MwenyeziMungu azidi kutulinda na kutuepusha na maradhi haya.

Hamad Rashid Mohamed (MBM)(MBLW).

Waziri wa Afya - Zanzibar.